


MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA ZA OKTOBA - DISEMBA, 2021 (VULI)



Dondoo muhimu za msimu wa mvua za Vuli kipindi cha Oktoba - Disemba, 2021

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mwelekeo wa msimu wa mvua za Vuli kipindi cha Oktoba - Disemba 2021, ushauri na tahadhari kwa wadau wa sekta mbalimbali kama vile kilimo na usalama wa chakula, mifugo na uvuvi, maliasili, wanyamapori na utalii, nishati na maji, usafirishaji (nchi kavu, kwenye maji na angani), mamlaka za miji, afya pamoja na menejimenti za maafa. Utabiri huu ni mahsusi kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka (Nyanda za juu kaskazini mashariki, Pwani ya kaskazini, Ukanda wa Ziwa Viktoria pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma). Kwa muhtasari, mwelekeo huo na athari zake unaonesha kuwa:

a) Mvua za Vuli, 2021

- i. Mvua za Vuli zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani na zinatarajiwa kuambatana na vipindi virefu vya ukavu katika maeneo mengi yanayopata mvua za Vuli.
- ii. Msimu wa Vuli unatarajiwa kuanza kwa kusuasua katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Oktoba 2021 ukiwa na mtawanyiko na muendelezo usioridhisha katika maeneo mengi.
- iii. Mbali na mvua za chini ya wastani hadi wastani zinazotarajiwa, vipindi vya joto kali kuliko kawaida vinatarajiwa katika msimu wa Vuli.

b) Athari zinazotarajiwa

- i. Upungufu wa unyevunyevu katika udongo unatarajiwa kujitokeza katika maeneo mengi.
- ii. Kujitokeza kwa magonjwa ya mlipuko, kutokana na upungufu wa maji safi na salama.
- iii. Upungufu wa malisho na maji unaweza kujitokeza hivyo kusababisha kujitokeza kwa migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.
- iv. Uwezekano wa kutokea matukio ya moto katika mapori na misitu, hivyo mamlaka husika zinashauriwa kupanga mikakati mahsusi ya kukabiliana na hali hiyo.

(I) MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA KIPINDI CHA OKTOBA - DISEMBA, 2021

Msimu wa mvua za Vuli ni mahsusi kwa maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), pwani ya kaskazini (kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, mikoa ya Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), Dar es Salaam na Tanga, pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), ukanda wa Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu na Mara) pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma (wilaya za Kibondo na Kakonko).

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa ilivyo kwa sasa na inavyotarajiwa katika kipindi chote cha msimu (kama inavyoelezwa katika kipengele cha III cha taarifa hii), kwa ujumla mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Hata hivyo, baadhi ya maeneo ya ukanda wa Ziwa Viktoria yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani. Msimu unatarajiwa kuanza kwa kusuasua na kuambatana na mtawanyiko wa mvua usioridhisha. Hata hivyo, vipindi vya ongezeko kidogo la mvua vinatarajiwa kujitokeza katika maeneo machache kwa kipindi cha mwezi Disemba, 2021.

Mbali na mvua za chini ya wastani hadi wastani zinazotarajiwa, vipindi vya joto kali kuliko kawaida vinatarajiwa katika msimu wa Vuli, hususan katika maeneo ya pwani ya kaskazini na nyanda za juu kaskazini mashariki.

1. *Kanda ya Ziwa Viktoria: (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Mara pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma (wilaya za Kibondo na Kakonko)):*


Mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani katika maeneo mengi ya mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, magharibi mwa mkoa wa Shinyanga pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma. Aidha, maeneo ya mikoa ya Simiyu, Mara na mashariki mwa mkoa wa Shinyanga yanatarajiwa kuwa na mvua za chini ya wastani hadi wastani. Mvua hizi zinatarajiwa kuanza wiki ya tatu ya mwezi Oktoba, 2021 na kuisha katika mwezi Januari, 2022.

2. Ukanda wa Pwani ya Kaskazini: (kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, mkoa ya Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), Dar es Salaam, Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):

Mvua zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi ya ukanda wa pwani ya kaskazini. Msimu unatarajiwa kuanza kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Oktoba, 2021. Aidha, katika mkoa wa Morogoro kuanza kwa msimu kunatarajiwa kuwa kwa kusuasua kutokana na kuwepo kwa vipindi vingi vya ukavu. Mvua katika ukanda wa pwani ya kaskazini zinatarajiwa kuisha katika mwezi Januari, 2022.

3. Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki: (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):

Mvua zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi ya Nyanda za juu Kaskazini Mashariki. Msimu utaanza kwa kusuasua katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Oktoba, 2021 na kutawaliwa na vipindi virefu vya ukavu, mtawanyiko na muendelezo usioridhisha katika maeneo mengi. Mvua zinatarajiwa kuisha katika wiki ya nne ya mwezi Disemba, 2021.



Angalizo:

Ingawa maeneo mengi yanatarajiwa kupata mvua za chini ya wastani hadi wastani, izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza yakajitokeza katika maeneo machache.

(II) ATHARI NA USHAURI

Taarifa ya athari na ushauri imeandaliwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kwa kushirikiana na wataalamu wa sekta husika katika mkutano wa wadau wa hali ya hewa uliofanyika tarehe 31 Agosti, 2021.

a) Kilimo na Usalama wa Chakula

Upungufu wa unyevunyevu katika udongo unatarajiwa kujitokeza katika maeneo mengi yanayopata mvua za vuli. Hata hivyo, upungufu zaidi wa unyevunyevu unatarajiwa katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini na ukanda wa pwani ya kaskazini ambapo hali hii inaweza kuathiri ukuaji wa mazao. Aidha, ongezeko la visumbufu vya mazao kama mchwa, viwavijeshi, panya na magonjwa vinatarajiwa kujitokeza katika msimu na hivyo kuathiri mazao na uzalishaji kwa ujumla. Hali kadhalika uzalishaji wa asali unatarajiwa kuathirika kutokana na upungufu wa maji na maua. Kwa upande wa kilimo cha mwani, zao hilo linaweza kuathirika kutokana na vipindi virefu vya ukavu vinavyotarajiwa.

Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu na mazao yanayoweza kukomaa ndani ya muda mfupi na yanayostahimili ukame. Aidha, wanashauriwa kutumia mbinu na teknolojia za kilimo himilivu za kuhifadhi maji na unyevunyevu wa udongo. Wakulima wazingatie kupata ushauri kutoka kwa maafisa ugani juu ya namna bora ya kuendesha kilimo kwa usalama wa chakula na lishe. Aidha mamlaka husika zinashauriwa kutoa elimu na ushauri kwa wakulima juu ya njia bora na namna ya kutumia kiwango kidogo cha mvua kinachotarajiwa pamoja na matumizi mazuri ya akiba ya chakula kilichopo.

b) Mifugo na Uvuvi

Upungufu wa mvua katika msimu unatarajiwa kuathiri upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo na upatikanaji wa chakula kwa ajili ya Samaki. Hali hii inatarajiwa kuathiri uzalishaji wa mifugo, mazao ya mifugo na samaki. Vile vile, baadhi ya magonjwa ya mifugo (yanayoenezwa na kupe pamoja na wadudu warukao) na samaki yanatarajiwa kupungua, lakini vifo vya wanyama kutokana na ukame na magonjwa nyemelezi yanatarajiwa kuongezeka. Hali kadhalika kutokana na upungufu wa malisho na maji kuna uwezekano wa migogoro kujitokeza baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Jamii inashauriwa kuweka mpango mzuri wa matumizi na uhifadhi wa maji na malisho, kufuga kibiashara na kupunguza mifugo kulingana na eneo husika la malisho. Aidha,

wafugaji na wavuvi wanashauriwa watumie taarifa za utabiri wa hali ya hewa na kuzingatia ushauri wa maafisa ugani.

c) Utalii na Wanyamapori

Hali ya malisho na maji kwa wanyamapori inatarajiwa kupungua hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za chini ya wastani hadi wastani. Hali hii inaweza kudhoofisha afya za wanyamapori. Hata hivyo, hali ya joto inatarajiwa kusababisha kuongezeka kwa magonjwa ya wanyamapori. Hivyo, mamlaka husika zinashauriwa kuchukua hatua stahiki dhidi ya magonjwa ya wanyamapori.

d) Usafiri na Usafirishaji

Maeneo mengi yanatarajiwa kupata mvua za chini ya wastani hadi wastani, hivyo sekta ya usafiri na usafirishaji hususan usafiri wa ardhini inaweza kunufaika kutokana na vipindi vya ukavu vinavyoweza kujitokeza. Hata hivyo, inashauriwa kuwa mipango ya uboreshaji wa miundombinu ifanyike kwa kuzingatia taarifa za utabiri wa hali ya hewa katika eneo husika.

e) Nishati, Maji na Madini

Upungufu wa kina cha maji katika mito, mabwawa na hifadhi ya maji ardhini unatarajiwa kujitokeza hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za chini ya wastani. Hali hii inaweza kupunguza upatikanaji wa maji kwa matumizi mbalimbali. Uzalishaji wa madini (hususan dhahabu kwa wachimbaji wadogo) na nishati ya umeme utokanao na maji unaweza kuathirika (unaweza kupungua). Watumiaji katika sekta ya maji wanaweza kuathirika na kupelekea migogoro kati ya watumiaji wakubwa na wadogo. Hata hivyo, utekelezaji wa miradi ya umeme, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi unatarajiwa kuendelea vizuri. Aidha, wadau wanasisitizwa kuzingatia matumizi endelevu ya maji katika shughuli za kuchakata madini, uzalishaji wa umeme, matumizi viwandani na majumbani.

f) Mamlaka za Miji

Kutokana na matarajio ya upungufu wa mvua, mamlaka za miji zinashauriwa kutumia fursa hiyo kuboresha miundombinu kuhakikisha kuwa mifumo na njia za kupitisha maji zinafanya kazi katika kiwango kinachostahili. Kwa kuzingatia vipindi vifupi vya mvua kubwa

vinavyoweza kujitokeza, Mamlaka za miji zinashauriwa kuboresha miundombinu ili kupunguza athari za mafuriko ya ghafla.

g) Sekta ya Afya

Katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za chini ya wastani hadi wastani upungufu wa upatikanaji wa maji safi na salama unaweza kujitokeza na kusababisha mlipuko wa magojwa. Mamlaka za afya zinashauriwa kuchukua hatua stahiki kupunguza athari hasi, ikiwa ni pamoja na kuhimiza wananchi kutibu maji kabla ya kutumia, kunywa maji safi, salama, na ya kutosha ili kuepuka upungufu wa maji mwilini. Hata hivyo, msisitizo unatolewa kwa mamlaka husika kutoa elimu ya afya kwa wananchi na kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

h) Sekta Binafsi

Shughuli za kibiashara zinazohusisha hali ya hewa zinaweza kuathirika kutokana na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji kutokana na matumizi makubwa ya nishati katika uhifadhi wa mazao tete na bidhaa. Mvua za chini ya wastani zinaweza kusababisha kuathirika kwa ubora wa miti ya nguzo na mbao.

Wadau wa Sekta binafsi wanashauriwa kushirikiana na wataalamu mbalimbali ikiwemo wataalam wa hali ya hewa ili kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza. Hatua za kupunguza matawi ya miti ya nguzo na mbao zitekelezwe mara kwa mara. Taasisi za Benki na Bima zinashauriwa kuandaa na kutoa huduma mahususi kwa wadau ili kujenga ustahimilivu katika biashara.

i) Menejimenti za Maafa

Katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua chini ya wastani hadi wastani, madhara yanavyoweza kujitokeza ni pamoja na upungufu wa chakula, malisho ya mifugo na maji. Mamlaka husika zinashauriwa kushirikiana na kuhakikisha uwepo wa usalama wa chakula, malisho ya mifugo, maji na kutoa miongozo ya namna ya kukabiliana na maafa ili kuzuia na kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

j) Vyombo vya habari

Vyombo vya habari vinashauriwa kufuatilia, kupata na kusambaza taarifa sahihi za mwenendo wa msimu wa Vuli pamoja na taarifa zilizo huishwa za hali ya hewa kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).

Wanahabari wanashauriwa kutafuta na kutumia ushauri wa kisekta kutoka kwa watoa taarifa wa sekta mbalimbali zinazotumia taarifa za hali ya hewa. Pia kuandaa na kusambaza makala na taarifa za tahadhari za kisekta kwa kutumia lugha nyepesi kwa lengo la kuhabarisha na kuelimisha jamii ipasavyo juu ya matumizi ya utabiri wa hali ya hewa katika kupunguza athari za hali mbaya ya hewa.

(III) MIFUMO YA HALI YA HEWA

Joto la bahari la wastani linatarajiwa katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi na joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi. Hali hii inatarajiwa kusababisha upungufu wa upepo wenye unyevunyevu kuelekea katika maeneo ya Pwani ya nchi. Matukio ya migandamizo midogo ya hewa katika eneo la Kusini magharibi mwa Bahari ya Hindi yanatarajiwa kusababisha kuhama kwa haraka kwa ukanda mvua, ITCZ, kuelekea sehemu za kusini mwa nchi.

Kwa upande mwingine, joto la bahari la juu ya wastani hadi wastani linatarajiwa katika bahari ya Atlantiki karibu na Pwani ya Angola, hivyo kupunguza msukumo wa upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo kuelekea katika maeneo ya nchi ya Tanzania. Aidha, eneo la kati la kitropikali katika bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuwa na joto la chini ya wastani, hivyo kuashiria uwepo wa La Nina hafifu itakayochangia katika upungufu wa mvua katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka.

Katika kipindi cha Msimu wa vuli 2021, kukosekana kwa msukumo wa kutosha wa upepo kunatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi, hivyo kufifisha msimu wa mvua za vuli. Aidha upepo hafifu wa matlai katika tabaka la chini la anga katika eneo la kaskazini mwa Congo unatarajiwa kupunguza mvua katika maeneo ya kaskazini magharibi mwa nchi.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendeleo kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.

Mwelekeo wa mvua uliotolewa hapa umezingatia zaidi kipindi cha msimu (miezi mitatu) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya mvua na mabadiliko ya muda mfupi katika maeneo madogo vitazingatiwa katika uchambuzi wa utabiri wa muda wa kati na mfupi. Watumiaji wa taarifa za utabiri huu wanashauriwa pia kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10 pamoja na mwezi kama unavyotolewa na Mamlaka ya hali ya Hewa Tanzania.

Mamlaka ya hali ya hewa Tanzania itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa mirejesho ya mwelekeo wa mvua nchini kadri inavyohitajika. Aidha, wadau wanashauriwa kuwasiliana na Mamlaka ili kupata taarifa mahsusi za utabiri wa msimu ili kukidhi mahitaji maalum katika sekta zao.

Imetolewa Tarehe 02 Septemba, 2021

Na: Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania: